**HOTUBA YA KATIBU MKUU KIONGOZI KATIKA UFUNGUZI WA MAFUNZO YA MAADILI KWA WATENDAJI WAKUU WA TAASISI NA MASHIRIKA YA UMMA, YATAKAYOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA WAKALA WA MAJENGO TANZANIA (TBA), TAREHE 06/04/2016**

---

**Mheshimiwa Jaji (Mst.) Salome S. Kaganda,**
**Kamishna wa Maadili;**

**Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma;**

**Katibu wa Sekretarieti ya Maadili eneo la Viongozi wa Utumishi wa Umma;**

**Katibu wa Sekretarieti ya Maadili eneo la Viongozi wa Siasa;**

**Watumishi wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;**

**Wanahabari;**

**Wageni Waalikwa;**

**Mabibi na Mabwana.**

*Habari za Asubuhi.*

Nianze kwa kukushukuru, Mheshimiwa Kamishna wa Maadili na Sekretarieti ya Maadili kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika Mafunzo haya ya Maadili yaliyowalenga Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma. Naipongeza Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kuendeleza mafunzo haya muhimu, ambayo yalikwishatolewa kwa Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri; Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu; Wenza wa Viongozi wa Umma na sasa yanatolewa kwa Watendaji Wakuu wa Taasisi

na Mashirika ya Umma. Binafsi nashukuru kwamba mafunzo haya ya leo yamenipa pia fursa ya kukutana na Watendaji Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma kwa mara ya kwanza tangu nilipoteuliwa katika nafasi ya Katibu Mkuu Kiongozi.

Jitihada hizi za Serikali kutoa mafunzo haya kupitia Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni kielelezo dhahiri cha dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuhakikisha kuwa suala la maadili, uadilifu na uwajibikaji linaeleweka vilivyo kwa wadau wote wa sekta ya umma na sekta binafsi na uelewa huo ni sharti uwe endelevu.

**Ndugu Washiriki,**

Kama mnavyofahamu Maadili ya Taifa ni nguzo muhimu katika ufanikishaji wa mipango ya maendeleo ya nchi yoyote duniani. Upo umuhimu wa kuhakikisha kuwa tunalinda na kujenga utamaduni wa kuzingatia maadili katika Taasisi na Mashirika tunayoyaongoza na jamii kwa ujumla. Maadili yana umuhimu mkubwa katika utawala na maendeleo ya nchi, kwani:

- Yanasaidia kujenga imani ya wananchi kwa Viongozi na Serikali kwa ujumla;
- Yanasaidia kuhakikisha kuwa Rasilimali za umma zinatumika kwa maslahi ya wote;
- Yanasaidia kuongeza tija na thamani ya huduma zinazotolewa na Serikali;
- Yanasaidia kudhibiti mianya ya vitendo vya rushwa;

- Yanasaidia kujenga ujasiri wa kusimamia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma;

- Yanawezesha wananchi, Viongozi na Watumishi wa Umma kutoa mchango mkubwa na wa haraka katika utekelezaji wa maendeleo ya nchi;

- Yanaepusha utata wa maamuzi au mgongano wa maslahi;

- Yanawezesha kuweka mazingira chanya ya uwekezaji;

- Yanajenga na kudumisha amani, utulivu, kuheshimiana na umoja wa kitaifa; na

- Yanaondoa hulka ya ubinafsi kwa Viongozi.

Wote tunajua kuwa suala la utovu wa maadili katika nchi yetu limekuwa likitajwa sana katika miaka ya nyuma, ndio maana Serikali ya Awamu ya Tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imedhamiria kwa dhati kabisa kulivalia njuga suala hili, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha inachukua hatua mbalimbali za uwajibikaji kwa watendaji wote wanaotuhumiwa kukiuka maadili, wakiwemo wanaojihusisha na vitendo vya dhuluma, rushwa, ufisadi na kutumia madaraka yao kujinufaisha.

Ni vyema ieleweke hata hivyo kuwa hatua hizi za Serikali, maarufu kama "utumbuaji majipu", zinakusudia kuondoa kero zilizopo na kurejesha nidhamu na maadili yaliyojengeka katika misingi ya utawala bora katika ngazi zote nchini. Hatua hizi ni mithili ya tiba ya gonjwa sugu ambalo lazima litibiwe ili kuleta ahueni kwa mtu aliyeathirika nalo. **Ni hatua za kufa na kupona zisizokwepeka**.

Ninyi mkiwa kama walezi wa maadili katika Taasisi zenu, mnapaswa kuhakikisha kwamba mmeelimika vya kutosha kuhusu Sheria na Kanuni za Utumishi kuhusu maadili, na kuwasimamia watumishi walio chini yenu kwa umakini zaidi ili kuhakikisha maadili na uadilifu vinakua na kudumishwa.

Naamini mtapata uelewa mzuri zaidi wa masuala hayo baada ya Mafunzo haya ambayo yanalenga zaidi katika kinga (*prevention*) badala ya kuponya (*cure*). Naomba msisite kuchangia na kuuliza maswali kwa lengo la kuongeza uelewa kwani mnao muda wa kutosha kujadili kwa pamoja mada zitakazowasilishwa na watendaji wa Sekretarieti ya Maadili.

**Ndugu Washiriki,**

Imekuwepo dhana potofu katika jamii kwamba tatizo la rushwa na utovu wa maadili liko katika Sekta ya Umma peke yake, suala ambalo sio sahihi hata kidogo. Inafahamika bayana kwamba, vishawishi vingi na vitendo vya utoaji wa rushwa unafanywa na Sekta Binafsi. Hivyo mkakati wa mapambano dhidi ya rushwa na utovu wa maadili unatakiwa kuwa shirikishi (*inclusive*). Ndiyo maana, hata kabla ya Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani, Serikali ilikwishaanzisha utaratibu wa **Viongozi, Watumishi wa Umma na Sekta Binafsi** kutoa ahadi za kuzingatia misingi ya maadili na mapambano dhidi ya rushwa kupitia "**Hati ya Ahadi ya Uadilifu**" kwa makundi yote hayo matatu.

Napenda kusisitiza tena kuwa, jukumu la kukuza maadili nchini sio la mtu ama Taasisi moja, ni jukumu letu sote, kila mtu kwa nafasi aliyonayo katika jamii. Mathalan, wazazi wanawajibu wa malezi na makuzi kwa watoto wao; Taasisi za elimu zinawajibu wa makuzi ya wanafunzi wao; Taasisi za Dini zina wajibu wa malezi ya kiroho; Asasi za Kiraia zina wajibu wa kuishirikisha jamii na kushirikiana na Serikali katika kukuza maadili katika maeneo yao; Serikali ina wajibu wa kukuza na kusimamia maadili ya viongozi; na wake kwa waume wanawajibu kuwashirikisha wenza wao katika suala hili muhimu la maadili badala ya kuwabagua au kuwatumia kama maficho ya uovu wao. Mafanikio yetu katika kujenga utamaduni wa uadilifu nchini yatategemea namna tutakavyoimarisha ushirikiano wetu kufikia azma hiyo.

**Ndugu Washiriki,**

Ni lazima tutambue umuhimu wetu kama viongozi kuwa mfano wa kuigwa kwa watumishi tunaowaongoza na jamii yote kwa ujumla. Nawasihi

muwe walezi na walimu wazuri na wa kupigiwa mfano wa mwenendo mwema wa uadilifu ili wengine wafuate nyayo zetu. Kama viongozi wa Taasisi na Mashirika ya Umma mnapaswa kuepuka ukiukwaji wa namna yoyote wa maadili.

Badala yake, kama viongozi, tunawajibika kuwafunda watumishi tunaowaongoza kuhusu umuhimu wa maadili. Naishukuru Sekretarieti ya Maadili kwa kuonyesha utayari wa kuwawezesha katika suala hili kwa kuwafutia mafunzo haya. Wito wangu kwenu ni kwamba mafunzo haya ya leo yawe chachu ya mabadiliko katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku. Aidha, mkawe mabalozi wazuri katika Taasisi zetu ili hatimaye tujenge utumishi uliotukuka na kukuza heshima na imani ya wananchi wote kwa Serikali yao.

**Ndugu Washiriki,**

Wote tunafahamu dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuleta maendeleo ya kasi na endelevu kwa wananchi wake na kuondoa umaskini wa kila hali. Ili kufikia azma hiyo, Serikali inatekeleza mikakati ya kukusanya mapato, na kusisitiza umuhimu wa kubana matumizi na kuondoa yale yasiyo ya lazima. Badala ya kutumia fedha kwenye sherehe mbalimbali, Serikali inaelekeza fedha hizo katika kuimarisha huduma za kijamii. Badala ya kutumia fedha nyingi kwa ajili ya mikutano, semina na warsha za ndani na nje ya nchi, Serikali inaelekeza fedha hizo katika kutatua kero za wananchi na kuendeleza jitihada za kukuza uchumi ambao utawanufaisha wananchi wote. Ni dhahiri kuwa Serikali haitafanikisha mipango hii muhimu kama maadili na uadilifu havitazingatiwa.

Wote tunafahamu umuhimu wa Taasisi na Mashirika mnayoyaongoza. Tunafahamu kuwa Taasisi zetu zina mchango mkubwa katika kufanikisha mipango ya Serikali, hivyo ni lazima mtekeleze majukumu yenu kwa ufanisi na kuleta matokeo makubwa na yenye tija zaidi. Ni muhimu mkumbuke kuwa Taasisi na Mashirika mnayoyaongoza ni mali ya umma, hivyo umma unatarajia kuona matokeo chanya na yenye maslahi kwa umma huo. Linapokuja suala la kubana matumizi, ikumbukwe kuwa hili ni la kwetu wote; Serikali Kuu, Taasisi na Mashirika yote. Lazima tuweke mbele maslahi mapana ya Nchi; na lazima

tuepuke mgongano wa maslahi, hususan kwenye maamuzi kama vile manunuzi, ajira, kuchukua hatua za nidhamu n.k.

Ifahamike wazi kuwa Serikali haitamvumilia Kiongozi ama Mtumishi yeyote wa Umma atakayekiuka sheria, kanuni na miongozo inayolenga kukuza maadili na kuongeza ufanisi katika Utumishi wa Umma. Atakayeihujumu nchi atachukuliwa hatua; atakayetumia madaraka aliyokabidhiwa kujinufaisha yeye binafsi au familia au marafiki zake atachukuliwa hatua, na atakayekiuka maadili yaliyowekwa atashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria.

**Ndugu Washiriki na Wanahabari,**

Kabla sijahitimisha hotuba yangu nichukue fursa hii kushukuru Shirika la USAID la Marekani kwa kushirikiana nasi katika ufanikishaji wa mafunzo haya kwa Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma kama ambavyo Shirika hili lilishiriki katika mafunzo mengine kama haya yaliyofanyika kwa Viongozi wengine. Yapo maeneo mengine mengi ambayo Shirika la USAID limetusaidia lakini kutokana na ufinyu wa muda sitayazungumzia leo.

**Ndugu Wanahabari**,

Nimezungumzia wajibu wetu sote kukuza maadili nchini. Nitumie fursa hii kuwakumbusha Wanahabari kuhusu umuhimu wa kutumia taaluma yenu vizuri katika kuelimisha wananchi na viongozi kuhusu maadili tunayoyazungumzia na kukemea bila hofu wala upendeleo maovu katika jamii yetu. Nawasihi tudumishe uzalendo na kujali maslahi ya nchi yetu.

Baada ya kusema haya, natamka sasa kuwa mafunzo haya ya maadili kwa Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma yamefunguliwa rasmi. **Nawatakia mafunzo mema na yenye tija**.

***Ahsanteni sana kwa kunisikiliza***